# HABARI na MATUKIO

Toleo Na. 33 | Tanzania Fertilizer Regulatory Authority | tfra_official | tfra_official | Desemba 2025

JARIDA LA KILA MWEZI LA MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA


# TFRA YAIBUKA MSHINDI WA TATU TUZO YAUBUNIFU WA MIFUMO



Mwenyekiti wa Bodi ya TFRA, Dkt. Anthony Diallo, akikabidhiwa tuzo ya ubunifu (Innovation Management Award) na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent, katika hafla fupi ya kusherekea mafanikio ya TFRA kushika Nafasi ya Tatu katika shindano la ubunifu lililofanyika nchini Eswatini tarehe 20 Desemba, 2025.


NDANI>>

TFRA YAWEZESHA VIJANA KUPATA MBOLEA MAKETE 4






ELIMU YA MATUMIZI SAHIHI YA PEMBEJEO ZA KILIMO YAIMARISHA WAKULIMA 6

# TFRA YAIBUKA MSHINDI WA TATU TUZO YAUBUNIFU WA MIFUMO



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Joel Laurent, akipokea tuzo ya ubunifu (Innovation Management Award) kutoka kwa Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi (TFRA) Victoria Elangwa, ikiwa ni mafanikio ya kushika nafasi ya tatu katika shindano la ubunifu wa mifumo lililofanyika nchini Eswatini tarehe 20 Desemba, 2025.

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), imeibuka mshindi wa nafasi ya tatu katika shindano la ubunifu (Innovation Management Award) uliochangia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

Tuzo hiyo imetolewa tarehe 4 Desemba, 2025, Siku ya kilele cha Mkutano wa 44 wa Mwaka, wa JUMUIYA ya Afrika ya Wataalamu wa USIMAMIZI wa Utawala katika utumishi wa Umma (AFRICA ASSOCIATION OF PUBLIC ADMINISTRATION MANAGEMENT AAPAM) uliofanyika Manzini, Eswatini kuanzia tarehe 2-5 Desemba.

Akiwasilisha mada katika mkutano huo, Victoria Elangwa, Mkurugenzi wa Huduma za Mamlaka alieleza kuwa, mfumo wa kidijitali wa Pembejeo za Ruzuku ulianza kutekelezwa msimu wa kilimo wa mwaka 2022/2023 kwa lengo la kuongeza ufanisi kwenye utoaji wa ruzuku nchini.

Aidha alibainisha kuwa, kufuatia ufanisi huo, kwa sasa mfumo unatumika na taasisi za Wizara ya Kilimo ikiwa ni pamoja na Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI), Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), Bodi ya Pamba Tanzania, Bodi ya Kahawa Tanzania na Bodi ya Korosho Tanzania kutokana na taarifa zinazojazwa na mkulima kukidhi mahitaji ya taasisi hizo.

Katika tuzo hizo, ambapo TFRA iliwakilishwa na meneja wa Kitengo cha TEHAMA Robert Mtendamema nchi mbalimbali kutoka bara la Afrika ziliwasilisha jumla ya mapendekezo 49 kutoka nchi mbalimbali barani Afrika yaliyoshindanishwa katika kipengele cha Ubunifu Bora wa Mwaka ambapo TANZANIA na Afrika ya Kusini Zilifungana katika nafasi ya tatu huku Zambia ikiibuka mshindi wa kwanza.

Pamoja na ushindani mkali na mchujo wa kina, TFRA imefanikiwa kujipatia nafasi hiyo ikiwa ni ushahidi wa ubunifu, ufanisi na mchango mkubwa wa mfumo huo katika kuboresha utekelezaji wa mpango wa pembejeo za ruzuku nchini.

# TFRA YAIBUKA MSHINDI WA TATU TUZO YAUBUNIFU WA MIFUMO




Tuzo ya mshindi wa nafasi ya tatu ambayo Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania imeshinda tarehe 4 Desemba, 2025, Siku ya kilele cha Mkutano wa 44 wa Mwaka, wa JUMUIYA ya Afrika ya Wataalamu wa USIMAMIZI wa Utawala katika utumishi wa Umma (AFRICA ASSOCIATION OF PUBLIC ADMINISTRATION MANAGEMENT AAPAM) uliofanyika Manzini, Eswatini kuanzia tarehe 2-5 Desemba.

# TFRA YAWEZESHA VIJANA KUPATA MBOLEA MAKETE

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent, ameuhakikishia umma kuwa mbolea ya kupandia zipo na zinaendelea kuingizwa nchini.

Anasema, tumeshuhudia ushushaji wa tani elfu arobaini za mbolea aina ya NPS Zink na TSP na kampuni ya mbolea ya OCP Tanzania na kueleza kuwa serikali kupitia Kampuni ya Mbolea Tanzania inatarajia kushusha tani 35,500 za BAT katika kipindi hiki hadi kufikia katikati ya mwezi januari.

Anatoa uhakika huo wakati wa halfa ya kukabidhi mbolea kwa vijana wakulima baada ya TFRA kwa kushirikiana na wadau wa tasnia ya mbolea wakiwemo Minjingu, ETG, ITRACOM, OCP, TFC, METL na wakala wa Mbolea Mtewele, Mhema Agrovert, na Jabir kuitikia wito wa kuwawezesha vijana kiuchumi kwa kukikusanya mifuko 320 ya mbolea na kuwakabidhi kama mitaji.

Aidha, Laurent amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuinua Sekta ya Kilimo kupitia Tasnia ya mbolea.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Makete, Mhe. Kissah A.Kasongwa, anasema ugawaji huo wa mbolea unakwenda kuacha tabasamu miongoni mwa vijana wanaopokea msaada huo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent, akizungumza katika hafla ya ugawaji wa mbolea kwa wakulima wa Wilaya ya Makete, Mkoa wa Njombe, tarehe 16 Desemba, 2025.

Kwa niaba ya vijana na watu wenye ulemavu, Noadi Tweve anashukuru kwa msaada wa pembejeo waliopewa na kuhamasisha wilaya nyingine kuiga mfano wa Makete kwa kuwashirikisha vijana na watu wenye mahitaji maalum katika miradi ya kilimo, alibainisha kwamba jitihada hizo zitadumu ndani ya mioyo ya vijana walionufaika.




Mkuu wa Wilaya ya Makete, Mhe. Kissa A. Kasongwa, Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, na Mkurugenzi Mkuu wa TFC, Samuel Mshote, wakiwa katika picha ya pamoja na vijana waliogawiwa mbolea kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi kupitia kilimo, Wilaya ya Makete, Mkoa wa Njombe, tarehe16 Desemba 2025.

# TFRA YAWEZESHA VIJANA KUPATA MBOLEA MAKETE



Kwa niaba ya vijana na watu wenye ulemavu, Noadi Tweve akitoa shukrani kwa wadau wote waliochangia upatikanaji wa mbolea, katika hafla iliyofanyika Makete, Mkoa wa Njombe, tarehe 16 Desemba, 2025.



Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, akikabidhi mbolea kwa wakulima wa Wilaya ya Makete, Mkoa wa Njombe, tarehe16 Desemba, 2025, katika juhudi za kuwawezesha vijana kiuchumi kupitia kilimo.



Mkuu wa Wilaya ya Makete, Mhe.Kissa A. Kasongwa, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent, na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Mbolea Tanzania(TFC), Samuel Mshote, wakikata utepe wakati wa uzinduzi wa zoezi la ugawaji wa mbolea Wilaya ya Makete, Mkoa wa Njombe, tarehe16 Desemba, 2025.

# ELIMU YA MATUMIZI SAHIHI YA PEMBEJEO ZA KILIMO YAIMARISHA WAKULIMA



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent, akikagua hali ya upatikanaji wa mbolea katika ghala la OCP Halmashauri ya Mji wa Makambako, mkoani Njombe.

Elimu ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo ikiwemo mbolea imewawezesha wakulima nchini kujiandaa kununua na kutumia mbolea kulingana na mahitaji halisi ya udongo na zao husika na hivyo kusaidia kuongeza tija mashambani pamoja na kupunguza gharama zisizo za lazima kwa mkulima.

Kauli hiyo imetolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent, tarehe 17 Desemba, 2025, wakati wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya mamlaka ya kukagua na kuhakikisha upatikanaji wa mbolea kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa uliofanyika katika Halmashauri ya Mji wa Makambako, mkoani Njombe.

Akizungumza katika ghala la kampuni ya OCP Tanzania Joel anawasisitiza wakulima kutojihusisha na ununuzi wa mbolea nje ya mfumo wa ruzuku na kueleza mbolea zote zinapatikana kupitia mfumo huo na zinawafikia wakulima kwa bei elekezi.

Aidha, Afisa Udhibiti Ubora wa TFRA, Bw. Heneriko Renatus, alisema Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na taasisi zake ikiwemo TFRA inaendelea kutoa elimu kwa wakulima kupitia kampeni ya "Mali shambani" inayolenga kuwajengea uwezo wakulima katika kuboresha shughuli zao za kilimo.

Anaeleza kuwa, kupitia kampeni hiyo wakulima wanahimizwa kutumia lishe linganifu kwa viwango sahihi katika hatua za kupandia, kukuzia na kuzalishia, ili kuhakikisha mimea inapata virutubisho kwa wakati unaofaa.

Kwa upande wake, Meneja wa OCP Makambako, Bw. Charles Modest, anasema kwa sasa ghala la kampuni hiyo lina tani 3,000 za mbolea na limepokea tani 2,000 nyingine za mbolea za kupandia aina ya TSP na NPSZN, zitakazosambazwa kwa mawakala pamoja na wakulima wa Mkoa wa Njombe na wilaya zake.

# WAKULIMA ZAIDI YA 1,000 IGUNGA WAPATA ELIMU YA MATUMIZI SAHIHI YA MBOLEA

WAKULIMA zaidi ya 1,000 kutoka vijiji vya Sungwizi, Nkinga na Simbo, vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Igunga mkoani Singida, wameipongeza Serikali kwa kuwafikia na kuwapatia elimu kuhusu matumizi sahihi ya mbolea na mbegu bora, hatua inayolenga kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao.

Wakulima hao wamepatiwa mafunzo kwa nyakati tofauti kuanzia Desemba 5 hadi 7, 2025, kupitia Kampeni ya Mali Shambani, yaliyotolewa na wataalamu kutoka Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) pamoja na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA).

Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea wakulima uelewa wa kitaalamu kuhusu matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo, ikiwemo mbolea na mbegu bora, ili kuongeza uzalishaji, kuboresha ubora wa mazao na kupunguza gharama zisizo za lazima mashambani.

Wilaya ya Igunga ni miongoni mwa maeneo yanayozalisha kwa wingi mazao mbalimbali yakiwemo pamba, choroko, dengu, mahindi, karanga na mpunga, hivyo elimu hiyo inatarajiwa kuwa chachu ya kuimarisha uzalishaji na kuongeza kipato cha wakulima katika eneo hilo.



Afisa Kilimo Mkuu Mwandamizi kutoka Wizara ya Kilimo Alphonce Mwiru akizungumza na wakulima wa Halmashauri ya Igunga mkoani Singida kuhusu matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo ili kuongeza tija na uzalishaji mashambani.



Wakulima wa Wilaya ya igunga Kijiji cha Sungwizi walifuatilia mafunzo ya matumizi sahihi ya mbolea na mbegu bora yaliyotolewa kupitia Kampeni ya Mali Shambani.

# ELIMU YA MATUMIZI SAHIHI YA PEMBEJEO ZA KILIMO YAIMARISHA WAKULIMA



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent, akikagua hali ya upatikanaji wa mbolea katika ghala la OCP Halmashauri ya Mji wa Makambako, mkoani Njombe.



Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA , Joel Laurent (katikati) akipeana mkono na Zakayo Mwipunyinywe, Mkurugenzi wa Zakayo Agrovet (wakala wa usambazaji wa mbolea), wakati wa ukaguzi wa upatikanaji wa mbolea Makambako, mkoani Njombe. Kulia kwake ni Oraph Stanley Mhema, Wakala wa Kampuni ya Mhema Agrovert.

# TFRA Yatangaza Mafunzo Bure ya Leseni za Uuzaji Mbolea kwa Wakulima Rorya

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imetoa tangazo la fursa ya mafunzo ya mbolea kwa wakulima na wananchi wanaotamani kuanzisha biashara ya mbolea katika vijiji vya Tatwe, Nyamusi na Panyakoo vilivyopo Wilaya ya Rorya, mkoani Mara.

Akizungumza tarehe 11 Desemba 2025, akitekeleza kampeni ya Mali Shambani, Afisa Udhibiti Ubora Mwandamizi kutoka TFRA, Godwin Vedastus, alisema kuwa elimu hiyo ya mbolea inatolewa bure ikilenga kuongeza mawakala wa mbolea na hivyo kuwahakikishia wakulima upatikanaji wa mbolea karibu na makazi yao.



Wakulima wa kijiji cha Tatwe kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Rorya Mkoa wa Mara wakifuatilia mafunzo ya matumizi sahihi ya mbolea ikiwa ni utekelezaji wa kampeni ya Mali Shambani inayoendelea mkoani humo tarehe 11 Desemba, 2025.

"Mamlaka inatoa mafunzo haya bure ili kumsaidia mkulima apate mbolea kwa urahisi. Mtu yeyote anayehitaji kuingia katika biashara ya mbolea anakaribishwa kupata leseni bila gharama," anasema Vedastus.

Kwa upande wake, Afisa Masoko kutoka Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Shafi Omary, anasema kuwa, kampuni hiyo imepunguza masharti ya usajili kwa mawakala wapya ambapo inasajili mawakala kwa kianzio cha mifuko 20 pekee lengo likiwa ni kupanua mtandao wa usambazaji wa mbolea nchini.



Afisa Kilimo kutoka Chama cha Msingi cha Wakulima wa Mara Cooperative Union (WAMACU) LTD, Daniel Chacha akieleza fursa mbalimbali za kilimo ikiwemo uuzaji wa pembejeo za kilimo kwa wakulima wa kijiji cha Nyamusi ili washiriki katika kusogeza huduma hiyo karibu na wakulima tarehe 11 Desemba, 2025.



Mkulima wa kijiji cha Panyakoo kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Rorya mkoani Mara akielezea aina mbalimbali za mbolea ya Minjingu Fertilizer na anavyozitumia kuleta tija kwenye kilimo hasa cha mahindi tarehe 11 Desemba, 2025.

Naye Afisa Mawasiliano na Masoko wa Minjingu Fertilizers Ltd, Kisuma Mapunda, anaeleza kuwa, kampuni hiyo imerahisisha masharti kwa wakulima na vijana wanaotaka kuingia katika biashara ya mbolea.

"Kwa Minjingu, mtu anaweza kuwa wakala kwa kianzio cha kuanzia shilingi 500,000 tu. Tumepunguza gharama ili kuwapa nafasi wakulima na vijana kujiendeleza kiuchumi," alisema Mapunda.

Kupitia fursa hizi, wakulima wa Rorya wanatarajiwa kunufaika na upatikanaji wa mbolea kwa urahisi zaidi, huku vijana na wajasiriamali wakifunguliwa milango ya kujiendeleza kiuchumi. Hatua hii inatarajiwa kuongeza idadi ya mawakala na kuboresha mnyororo mzima wa usambazaji wa pembejeo za kilimo katika mkoa wa Mara.

# Mali Shambani yatajwa Suluhisho la Changamoto za wakulima Mara

Wakulima wa Kijiji cha Susuni Wilaya ya Tarime mkoani Mara, wamejengewa uwezo kuhusu matumizi sahihi ya mbolea baada ya kupatiwa mafunzo kupitia kampeni ya Mali Shambani inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo na taasisi zake.

Akieleza lengo la mafunzo hayo tarehe 12 Desemba, 2025, Samson Poneja, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Maendeleo ya Mazao, alisema lengo kuu ni kuwajengea wakulima uwezo wa kutambua kanuni bora za kilimo ikiwemo kanuni za matumizi sahihi ya mbolea, Viuatilifu na mbegu bora.

Alibainisha kuwa, changamoto kubwa imekuwa ni wakulima kutumia mbolea bila kupima afya ya udongo wao hali inayosababisha kutokupata matokeo mazuri shambani.

Kwa upande wake, Godwin Vedastus, Afisa Udhibiti Ubora Mwandamizi kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), aliwahimiza wakulima kuhakikisha wanazingatia kanuni 4 za matumizi sahihi ya mbolea kwa kuzingatia kupima afya ya udongo ili kuchagua mbolea kulingana na virutubisho vilivyopungua kwenye udongo.



Afisa Udhibiti Ubora Mwandamizi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Godwin Vedastus akitoa elimu ya mbolea kwa wakulima wa kijiji cha Susuni kilichopo Wilaya ya Tarime Mkoani Mara tarehe 12 Desemba,2025.



Mkulima kutoka kijiji cha Susuni kilichopo Halmshauri ya Wilaya ya Tarime mkoani Mara Joseph Marwa akielezea namna anavyotumia mbolea katika cha bustani za mbogamboga na jinsi anavyopata mavuno mengi wakati wa utekelezaji kampeni ya Mali shambani tarehe 12 Desemba, 2025.



Wakulima wa kijiji cha Susuni kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Tarime Mkoani Simiyu wakifuatilia mafunzo ya matumizi sahihi ya mbolea tarehe 12 Desemba, 2025 ikiwa ni utekelezaji wa kampeni ya Mali Shambani yenye lengo la kutoa elimu ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo.

Aidha, Mkulima Joseph Marwa alisema wamefarijika kwa kupatiwa elimu hiyo hususan katika kuchagua mbolea kulingana na aina ya mazao na upungufu uliopo kwenye udongo na kukiri elimu hiyo imekuwa chachu na kuwapa matumaini mapya kuelekea msimu wa kilimo wa 2025/2026.

Uelewa huu mpya umeongeza matumaini kwa wakulima ambao sasa wanatarajia kuongeza uzalishaji kwa kuchagua mbolea kwa usahihi kulingana na mahitaji ya udongo kwani sasa watapima udongo ili kujua virutubisho vinavyohitajika kwenye mashamba yao.

# Siri ya Mafanikio Shambani ni Mbolea



Wakulima wa kijiji cha Masewa kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi Mkoani Simiyu wakifuatilia mafunzo ya matumizi sahihi ya mbolea tarehe 6 Desemba, 2025 ikiwa ni utekelezaji wa kampeni ya Mali Shambani yenye lengo la kutoa elimu ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo.

Wakulima wa Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu wanaendelea kuthibitisha kwa vitendo kwamba siri ya mavuno mengi imo kwenye uzingativu wa matumizi sahihi ya mbolea.

Katika mashamba ambayo kwa miaka mingi yalikuwa yakitegemea bahati na hali ya hewa, leo hii mbolea imekuwa nguzo inayowapa matumaini kwa kuongeza tija na msukumo wa kuendelea kulima kwa bidii.

Hayo yamebainika wakati wa kampeni maalum ya Mali Shambani, inayolenga kuwafikia wakulima moja kwa moja na kuwapa mbinu bora za kuongeza uzalishaji ikitekelezwa na Wizara ya Kilimo na Taasisi zake mkoani humo kama sehemu ya kuwaandaa wakulima kuelekea msimu wa kilimo wa mwaka 2025/2026.

Miongoni mwa walioguswa zaidi na kampeni hiyo ni Magesa Nyamogo, mkulima wa pamba kutoka kijiji cha Masewa aliyeelezea mafanikio yake ya sasa kuwa si mazingaombwe bali ni matokeo ya kutumia mbolea kwa usahihi.

Alisema, msimu huu amevuna kilo 1,700 za pamba kwa ekari, ikiwa ni ongezeko maradufu ikilinganishwa na misimu ya nyuma ambapo alikuwa akivuna kilo 250 hadi 400 ongezeko lililompa nguvu ya kuendelea kuboresha shughuli za kilimo na kuiona kesho kwa matumaini makubwa kupitia kilimo.

Magesa alieleza kuwa, hakusita kujaribu kutumia mbolea kwenye zao la alizeti na matokeo yalikuwa ya kushangaza. Anaeleza kuwa alizeti ilistawi vizuri, ikavutia machoni na kumpa mavuno mengi zaidi ya miaka yote aliyolima bila mbolea. Kwa yeye, mbolea imekuwa "mwalimu mpya" wa kumfundisha kilimo chenye tija.

Shuhuda za wakulima hazikuishia kwa Magesa pekee, mkulima wa mahindi Gibu Lushuludo, kutoka kijiji cha Gilya, anaeleza kuwa kupitia mafunzo ya matumizi sahihi ya mbolea, ameshuhudia mabadiliko makubwa kwenye uzalishaji wake huku akishuhudia mavuno kuongezeka maradufu, hatua iliyompa uwezo wa kuzalisha mahindi ya kutosha kwa ajili ya familia na pia kwa ajili ya biashara.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Maendeleo ya Mazao, Samson Poneja, alisisitiza kuwa matumizi sahihi ya mbolea ndiyo dira ya kufikia malengo ya Ajenda 10/30: Kilimo ni biashara kwani wakulima watalima na kuvuna mazao mengi yatakayowafaa kwa chakula pamoja na biashara.

Alibainisha kuwa, serikali inaendelea kuhimiza wakulima kutumia mbolea kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo, ili kufikia lengo la matumizi ya kilo 40–50 za virutubisho vya mbolea kwa ekari kiwango kinachotajwa kuwa msingi wa mapinduzi ya kilimo Afrika.

# Siri ya Mafanikio Shambani ni Mbolea



Wakulima wa kijiji cha Banemhi kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi Mkoani Simiyu wakifuatilia mafunzo ya matumizi sahihi ya mbolea tarehe 6 Desemba, 2025 ikiwa ni utekelezaji wa kampeni ya Mali Shambani yenye lengo la kutoa elimu ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo.



Wakulima wa kijiji cha Gilya kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi Mkoani Simiyu wakifuatilia mafunzo ya matumizi sahihi ya mbolea tarehe 6 Desemba, 2025 ikiwa ni utekelezaji wa kampeni ya Mali Shambani yenye lengo la kutoa elimu ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo.

# ELIMU YA MBOLEA YABADILI MAZAMO WAKULIMA MEATU



Mkulima wa kijiji cha Mandoya kilichopo Halmsahauri ya Wilaya ya Meatu Mkoani Simiyu, Kobadi Makoye , akieleza namna anavyotumia mbolea ya samadi katika kilimo cha pamba wakati wa utekelezaji wa kampeni ya Mali shambani unaofanywa baina ya Wizara ya Kilimo na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), tarehe 4 Desemba , 2025.

Wakulima wilayani Meatu Mkoani Simiyu wamebadilisha mtazamo baada ya kupata mafunzo yaliyowapelekea kufahamu kuwa mbolea si chanzo cha uharibifu wa udongo, isipokuwa ni nyenzo muhimu ya kuuwezesha udongo kurudisha uhai wake na kuchochea uzalishaji.

Hayo yalibainishwa na wataalam wa kilimo wakati wa kampeni maalum ya Mali Shambani inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo na taasisi zake kuelekea msimu wa kilimo wa mwaka 2025/2026.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, Newaho Mkisi, alishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kundelea kuweka nguvu katika kuboresha sekta ya kilimo nchini hasa kwa kuweka ruzuku kwenye pembejeo za kilimo hususan mbolea na mbegu.

Mkisi amesema kuwa, mahitaji ya mbolea wilayani humo yameongezeka sana tofauti na ilivyokuwa miaka mitatu iliyopita. Ameeleza kuwa, sasa wakulima wanaelewa kuwa mbolea si adui wa udongo bali ni kirutubisho muhimu katika ukuaji wa mmea.

“Naipongeza TFRA kwa kuhakikisha mbolea zinazopatikana sokoni ni salama na zinakidhi mahitaji ya wakulima”, Mkisi aliongeza.

Kwa upande wake, Afisa Udhibiti Ubora Mwandamizi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Godwin Vedatus, alieleza kuwa, ili mimea ikue vizuri na kupata virutubisho muhimu, matumizi ya mbolea ni ya msingi. Alisema, udongo unapochoka, ni muhimu kurejesha virutubisho kwa kutumia mbolea ili kuimarisha ustawi wa mazao



Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Maendeleo ya Mazao, Wizara ya Kilimo, Samson Poneja akizungumza na wakulima wa kijiji cha Mwagwila kilichopo Halmsahuri ya Wilaya Meatu Mkoani Simiyu ikiwa ni utekelezaji wa Kampeni ya Mali Shambani ikilenga kuwaandaa wakulima kutumia pembejeo za kilimo kwa usahihi kuelekea msimu wa kilimo 2025/2026 ili kuongeza tija kwenye uzalishaji tarehe 4 Desemba, 2025.

“Mbolea haiharibu udongo. Kinyume chake, inauongezea virutubisho ambavyo mimea inahitaji ili kustawi kwa afya na uzalishaji wenye tija.” Aliongeza.

Aidha, mkulima Masanja Nkobadi ametoa wito kwa wakulima wenzake na kueleza kuwa dhana ya kwamba mbolea inaharibu udongo imekuwa ikiwadanganya kwa muda mrefu.

“Sisi Wasukuma tumekuwa tukijidanganya.Mimi nimetumia mbolea na nimepata mavuno mengi” Aliwasihi wakulima kutumia mbolea kwani inaongeza tija.



Mkurugenzi Msaidizi kutoka Idara ya Maendeleo ya Mazao Wizara ya Kilimo Samson Poneja akiwaelekeza wakulima wa kijiji cha Magwila kilichopo Halmsahuri ya Wilaya ya Meatu Mkoani Simiyu jinsi ya kufanya zoezi la T-Hakiki kujua ubora wa mbegu kupitia simu ya kiganjani tarehe 4 Desemba, 2025.

# MWENYEKITI WA BODI NA MENEJIMENTI YA TFRA WATEMBELEA KANDA YA KASKAZINI

Mwenyekiti wa Bodi Dkt. Anthony Diallo na menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) wamefanya ziara ya kikazi katika mikoa ya Manyara, Arusha, na Kilimanjaro kwa lengo la kujifunza na kuona namna bora ya Mamlaka kushirikiana na taasisi na wadau mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake pamoja na kujadili fursa zilizopo ili kuboresha tasnia ya mbolea na sekta ya kilimo kwa ujumla.

Katika ziara hiyo, timu ya TFRA ilitembelea sehemu mbalimbali ikiwemo viwanda vya Minjingu Mines & Fertilzer na Itracom Fertilizer Ltd vilivyopo Mkoa wa Manyara.

Kwa Mkoa wa Arusha timu ilitembelea kituo cha Keen Feeder (Foliar Fertilizer), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI-Selian), Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) na kupata fursa ya kutembelea Maabara na Benki ya Hifadhi ya Mbegu kwa ajili ya kujionea namna uhifadhi na usimamizi wa vinasaba vya mazao unavyofanyika.

Vilevile timu ya TFRA ilitembelea Mkoa wa Kilimanjaro katika ofisi ya Manispaa ya Moshi na kuzuru Skimu ya Mashamba ya Mpunga yaliopo Kaloleni-Moshi kujionea namna wakulima wanavyonufaika na mbolea za ruzuku lakini pia kuwapa elimu na ushauri kuhusiana na matumizi sahihi ya mbolea.

Mwisho, timu hiyo ilifanya majadiliano na (TPHPA, TARI na NM- AIST) kuhusu maeneo muhimu ya kufanya mashirikiano, ikiwemo urahisishaji wa huduma kwa wakulima, ukaguzi wa pembejeo, pamoja na tafiti katika kuhakikisha mbolea inayomfikia mkulima inakuwa na viwango vya ubora vilivyokusudiwa.








# TFRA YASHIRIKI MICHEZO YA SHIMUTA



Meneja Udhibiti Ubora na Majaribio, Schola Malila, aliibuka mshindi wa tatu katika awamu ya kwanza ya makundi kwenye michezo ya SHIMMUTA iliyofanyika mkoani Morogoro.

Imeelezwa kwamba ushiriki wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) katika michezo inayoandaliwa na Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma Taasisi na Makampuni Binafsi Tanzania (SHIMMUTA) Mwaka 2025 umeonesha mabadiliko na mwamko mkubwa kwa watumishi wa Mamlaka.

Hayo yamebainishwa na Mwenyekiti wa Michezo wa Mamlaka Frank Kapama mara baada ya kuhitimisha mashindano hayo yaliyotamatika mnamo tarehe 6 Desemba 2026 katika viwanja vya Jamhuri mkoani Morogoro.

Kapama ameeleza kuwa, TFRA ilipiga hatua kubwa zaidi kwa kupanua wigo wa ushiriki wake katika michezo ya SHIMMUTA iliyofanyika Mkoani Morogoro ambapo mbali na kuendelea kushiriki michezo ya ndani na mmoja wan je wa Kikapu wanaume, Taasisi iliongeza michezo ya nje mingine ikiwemo, mchezo wa pete wanawake na mpira wa kikapu wanaume, jambo lililoashiria ukuaji na ukomavu wa ushiriki wake katika michezo hiyo.

Aidha, washiriki katika mchezo wa riadha yaliyofanyika tarehe 3 Desemba 2025 waliendelea kuonesha ushindani, nidhamu na ari ya hali ya juu licha ya kuwa ni mara yao ya kwanza kushiriki mashindano ya mbio za SHIMMUTA.

Katika mbio za mita 100 (mzunguko wa kwanza), Meneja Udhibiti Ubora na Majaribio, Schola Mbalila alishiriki mbio za mita 100 huku Mtaalamu wa Maabara, Yohana Masalapilu akishiriki mbio za mita 800 na maafisa Udhibiti Ubora, Chrysanthus Funda na Raymond Konga wakishiriki na kufanikiwa kumaliza mbio ndefu za mita 5,000.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wanamichezo wa TFRA wanakiri kuwa mafanikio na ufanisi waliooneshwa katika mashindano hayo umechangiwa kwa kiasi kikubwa na juhudi za Menejimenti ya TFRA katika kuwawezesha kushiriki michezo ya SHIMMUTA, ikiwemo maandalizi, motisha na ushirikiano wa karibu.



Raymond Konga, Afisa Udhibiti Ubora kutoka TFRA, akifurahia baada ya kumaliza mbio za mita 400 katika michezo ya Shimmuta yaliyofanyika Mkoani Morogoro




Mtaalamu wa Maabara, Yohana Masalapilu, ameshika nafasi ya tano katika mbio za mita 800 kwenye michezo ya SHIMMUTA iliyofanyika Morogoro.




Wachezaji wa timu ya mpira wa pete ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) wakiwa katika picha ya pamoja kabla ya kuanza mchezo dhidi ya TFC (Wakala wa Huduma za Misitu), katika Mashindano ya SHIMMUTA yanayoendelea mkoani Morogoro.




Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji mbaye pia ni meneja Rasilimali Watu na Utawala wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), (kutoka kulia), Ibrahim Matovu, akiwa katika picha na watumishi wa Mamlaka walioshiriki michezo iliyoandaliwa na Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma, Taasisi na Kampuni Binafsi Tanzania (SHIMMUTA) mara baada ya hafla ya kufunga mashindano hayo yaliyofanyika katika viwanja vya Jamhuri mkoani Morogoro tarehe 6 Desemba 2025.



Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) wakiwa katika picha ya pamoja kabla ya kuanza mchezo dhidi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA), katika Mashindano ya SHIMMUTA yaliyofanyika kuanzia tarehe 23 Novemba hadi tarehe 6 Desemba, 2025 mkoani Morogoro.

# MATUKIO MBALIMBALI USHIRIKI WA MAMLAKA MICHEZO YA SHIMMUTA



Afisa Biashara kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Beatrice Bazazi, akicheza mchezo wa karata dhidi ya mchezaji kutoka Bohari ya Dawa (MSD), katika viwanja vya Bwalo mkoani Morogoro, tarehe 28 Novemba 2025.



Wachezaji wa timu ya mpira wa wavu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) wakiwa katika picha kabla ya mchezo dhidi ya Timu ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), katika viwanja vya Bwalo, Morogoro, tarehe 28 Novemba 2025. Aliyeshika mpira ni Calvin Mikuza, Mhandisi Ujenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA).

# MATUKIO MBALIMBALI USHIRIKI WA MAMLAKA MICHEZO YA SHIMMUTA



Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Adam Malima, akizungumza wakati wa kufunga mashindano ya SHIMMUTA yaliyofanyika katika Viwanja vya Jamhuri, Morogoro, tarehe 6 Desemba 2026.




Mwenyekiti wa Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma, Taasisi za Serikali na Kampuni Binafsi Tanzania (SHIMMUTA), Bi. Roselyne Massam, akizungumza wakati wa kufunga mashindano ya SHIMMUTA yaliyofanyika katika Viwanja vya Jamhuri, Morogoro, tarehe 6 Desemba 2025.